Hadithi: Atakayezua katika dini yetu hii, yale yasiyokuwemo, basi yatarejeshwa

Aina: Akida- Itikadi- . Majina na Hukumu. . Uzushi. .

عَنْ عَائِشَةَ رضي الله عنها قَالَتْ: قَالَ رَسُولُ اللهِ صلى الله عليه وسلم:

«مَنْ أَحْدَثَ فِي أَمْرِنَا هَذَا مَا لَيْسَ فِيهِ فَهُوَ رَدٌّ» متفق عليه. ولمسلم: «مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا فَهُوَ رَدٌّ».

[صحيح] - [متفق عليه] - [صحيح البخاري: 2697]

Kutoka kwa Aisha -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-:

"Atakayezua katika dini yetu hii, yale yasiyokuwemo, basi yatarejeshwa" Kaipokea Bukhari na Muslim. Na kutoka kwa Muslim: "Atakayefanya amali yoyote isiyokuwa na amri yetu, basi itarejeshwa".

[Sahihi] - [Wamekubaliana Bukhari na Muslim juu ya usahihi wake] - [Swahiih Al Bukhaariy - 2697]

Ufafanuzi

Anabainisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa atakayetunga au kubuni jambo katika dini au akafanya amali yoyote ambayo haikuelekezwa na dalili yoyote kutoka katika Qur'ani na Sunna, basi jambo hilo litarejeshwa kwa mfanyaji wake na halitokubaliwa mbele ya Allah.

Katika Faida za Hadithi

1. **Ibada zote zimejengeka juu ya yale yalikuja katika Qur'ani na Sunna, hatutakiwi kumuabudu Allah Mtukufu isipokuwa kwa sheria aliyoiweka na si kwa uzushi na mambo ya kutungwa.**
2. **Dini haiendi kwa rai na kutazama lipi zuri, bali inakwenda kwa kumfuata Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-.**
3. **Hadithi hii ni ushahidi wa kukamilika dini.**

4. **Uzushi ni kila kilichozushwa katika dini na hakikuwepo katika zama za Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- na Masahaba zake katika itikadi (Aqida) au kauli au amali yoyote.** ⚠️
5. **Hadithi hii ni msingi katika misingi ya Uislamu, nayo ni sawa na mzani kwa matendo, kama ambavyo kila amali ambayo haikukusudiwa kupata radhi za Allah Mtukufu, mfanyaji wake hana thawabu ndani yake, hivyo hivyo kila amali ambayo haitakuwa samabamba na yale aliyokuja nayo Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- basi hiyo itarejeshwa kwa mfanyaji wake.** ⚠️
6. **Uzushi uliokatazwa ni ule unaokuwa katika mambo ya dini na si ya kidunia.** ⚠️

Aina tofauti

- Akida- Itikadi- . Majina na Hukumu. . Uzushi.

عربي English اردو Español Indonesia ئۇيغۇرچە বাংলা Français Türkçe
Русский Bosanski සිංහල हिन्दी 中文 فارسی Tiếng Việt Tagalog Kurdî
Hausa Português മലയാളം తెలుగు தமிழ் မြန်မာ ไทย Deutsch 日本語
پښتو অসমীয়া Shqip Svenska አማርኛ Nederlands ગુજરાતી Кыргызча नेपाली
Yorùbá Lietuvių دری Српски Soomaali тоҷикӣ Kinyarwanda Română
Magyar Čeština Moore Malagasy Fulfulde Oromoo ಕನ್ನಡ Wolof Azərbaycan
O‘zbek Українська ქართული Македонски ភាសាខ្មែរ Bambara ਪੰਜਾਬੀ मराठी
Kirundi Yao Kurmancî Bahasa Melayu